

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



“Kilimani” Iringa Road,
S.L.P. 1175,
41101 DODOMA,
Barua Pepe: rbcddodoma@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

DODOMA – DISEMBA 01, 2020

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI
WANNE KUFUNGULIWA MASHTAKA 28

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 na sheria nyinginezo.

Leo tunawapatia taarifa za matukio mawili yafuatayo:

Kwanza, kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, leo Desemba 1, 2020 tutawafikisha Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma watu wanne na kuwafungulia mashauri mawili yenye jumla ya mashtaka ishirini na nane (28) yanayohusiana na vitendo vya rushwa na kughushi.

Shauri la kwanza la jinai litakuwa dhidi ya Bw. Aithan Lucas Chaula (61) aliyekuwa Afisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na Mratibu wa pembejeo za kilimo za ruzuku kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2015/16 na Bw. Michael Gervas Mpembwa (44) ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni ya Agro Business and General Supply iliyopewa uwakala wa kusambaza pembejeo za kilimo katika Kijiji cha Zajilwa wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma kwa msimu huo.

Watashtakiwa kwa makosa 25 ya kughushi kinyume na Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 ambapo uchunguzi wetu umeonyesha kwamba kati ya Januari na Agosti, 2016 walighushi nyaraka kuonyesha kwamba Wakala alisambaza pembejeo, zikiwemo mbegu za mahindi na mbolea, kwa wakulima wa Zajilwa na hivyo kustahili malipo ya shilingi milioni kumi na nne (14,000,000/=) huku wakifahamu kwamba ni uongo.

Shauri la pili linawahusisha Bw. Benedict Baraguyu Mazengo (58) aliyekuwa Mtendaji wa Kata ya Ntyuka Jijini Dodoma na Bw. Anderson Jonathan Mwaluko (48) aliyekuwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Chimalaa Jijini Dodoma ambao wanakabiliwa na mashtaka matatu ya Ubadhirifu kinyume na kifungu cha 28(1); Matumizi ya Nyaraka Kumdanganya Mwajiri kinyume na kifungu cha 22 vyote vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007; pamoja na Kughushi kinyume na Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

Uchunguzi wa TAKUKURU umeonyesha kwamba Juni, 2015 watuhumiwa walighushi na kutumia nyaraka zenye maelezo ya uongo zilizowawezesha kutoa benki shilingi milioni mbili laki tisa sabini na mbili mia tisa kumi na sita (2,972,916/=) ambazo badala ya kuzitumia kwa kazi iliyopangwa walizifanyia ubadhirifu.

Pili, TAKUKURU imefanikiwa kurejesha Serikalini shilingi milioni kumi na moja laki saba na elfu saba mia tisa ishirini na tatu (11,707,923/=) ambazo zililipwa kwenye akaunti ya benki ya Mtumishi marehemu kama mshahara kuanzia Oktoba, 2013 hadi Machi, 2016 kinyume na taratibu. Ufuatiliaji wa Ofisi yetu ya Kondo umewezesha fedha hizo kuokolewa.

Mwisho tunawakumbusha wana Dodoma hasa watumishi wa umma kwamba rushwa ni kosa la jinai, na jinai haifi hivyo tuhakikishe tunaenenda kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi na tujiepushe na vitendo vya rushwa. Hailipi.

Imetolewa na:

Sosthenes Kibwengo

Mkuu wa TAKUKURU (M) Dodoma